UNITED DEMOCRATIC PARTY

UDP

KATIBA

KATIBA YA CHAMA

CHA

UNITED DEMOCRATIC PARTY (UDP)

SEHEMU YA 1

KUUNDWA NA JINA

Kumeundwa chama cha siasa kitakachojulikana kama **"The United Democratic Party"** na kuandikishwa kwenye daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa chini ya kifungu cha vyama vya siasa cha mwaka 1992, au kifungu kingine chochote kile kitakachorekebisha au kubadilisha kifungu hiki. Chama hiki kitakuwa kikiitwa kwa ufupi **UDP.** Makao makuu ya chama yatakuwa Dar es Salaam.

UDP kitakuwa ni chama cha siasa chenye matawi yake kote katika Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, na kitakuwa kikipigania na kuendeleza Demokrasia. Umoja, Haki kwa watu wote, na kitajitahidi kuunda katika nchi ya Tanzania, serikali yenye misingi yake ya mfumo wa demokrasia, umoja, upendo, haki, furaha na matumaini ya maisha bora kwa watanzania wote, na ili kufanikisha kufikia malengo haya, chama kinajiwekea mipango na makusudi yafuatayo :-

SEHEMU YA 2

MIPANGO NA MAKUSUDI

Demokrasia

2.1.1 Kuendeleza aina ya serikali ya kidemokrasia yenye misingi ya haki kwa wengi, kuchagua kwa njia ya kura ya wote, na kwa wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa. Kwa kufanikisha hatua hizi, chama kitajishughulisha kujenga utamaduni wa kidemokrasia yenye misingi ya vyama vingi na watu

pia kuwakilishwa na wajumbe wa kujitegemea, pamoja na vyama vya raia.

2.1.2 Kuimarisha Bunge na serikali za mitaa, kwa kuimarisha mipango ya uchaguzi wenye kupendelea misingi ya utawala wa walio wengi, na kwa makusudi haya UDP itajitahidi kutunga sheria zenye kupendelea uchaguzi huru, na kufutilia mbali sheria zinazozuia watu kushiriki katika uchaguzi.

2.1.3 Kuleta Elimu ya Kidemokrasia kwa watu wote ili kujenga tabia ya kuelewa wajibu wao, kama watanzania. Kuimarisha utamaduni wa kidemokrasia, na kwa msimamo huu, UDP itaendeleza na kuimarisha mipango ya elimu ya demokrasia kwa ajili ya watu wote, na vyuo vyote vya elimu.

2.2 Umoja

2.2.1 Kudumisha amani na umoja kama ilivyo tabia ya Watanzania kihistoria, kwa kufuata siasa zinazolinda na kuendeleza haki na uhuru wa watu

binafsi na vikundi vya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na vile vya kijamii, siasa, uchumi, dini na utamaduni na hasa kwa kuzingatia :-

(a) Haki za kuunda chama au kuwa mfuasi wa chama chochote cha siasa,

(b) Haki za kumiliki mali.

(c) Haki za kumiliki ardhi.

(d) Haki za usawa mbele ya sheria.

(e) Uhuru wa kusafiri, kufikiri, kujieleza na kutoa au kupata habari.

(f) Uhuru wa kuabudu kwa njia yeyote ile.

(g) Uhuru wa kufanya kazi, na kulipwa ujira unaostahili chini ya mazingira yanayostahili.

(h) Uhuru wa kuendesha biashara halali.

(i) Uhuru wa kujikusanyia utajiri, na kuanzisha shughuli yoyote ile ya kuleta mafanikio.

(j) Uhuru wa kujitafutia raha katika maisha na katika kuyaendeleza haya, chama kitahakikisha kuwa haki hizi zinafungamanishwa katika katiba ya nchi kwa agizo kuwa haki kama hizi hazitavunjwa kamwe.

2.2.2 Kudumisha usalama wa nchi na haki zake kwa kujipatia mipaka yake kwa njia ya siasa ya kirafiki na mataifa ya nje kwa misingi ya heshima kwa wote. Kwa nia hii, UDP itaheshimu tangazo la ulimwengu la haki za binadamu pamoja na mikataba ya haki za binadamu za umoja wa nchi za kiafrika, na kuhakikisha umoja na ushirikiano kiuchumi, na kisiasa na nchi za afrika na zinginezo, wakati ule ule tukilinda maslahi ya nchi yetu.

2.2.3 Kuhakikisha kuweko kwa mashirika ya kidemokrasia ya ndani na nje ili kuendeleza hali nzuri ya maisha kwa raia, na kusaidia mipango hii

UDP itasaidia mashirika yanayotawaliwa na watu, kama vile vyama vya wafanyakazi, vyama vya biashara, vyama vya ushirika, mashirika ya maendeleo ya wananchi, mashirika ya kijamii na mashirika ya michezo.

2.3 Haki na Usawa

2.3.1 Kuleta na kuimarisha utawala wa sheria na kutenganisha mamlaka ya kutunga sheria uwe mbali na utawala wa mahakama. Kwa kuendeleza hii, UDP itahakikisha kujitegemea kwa matawi haya matatu ya mamlaka na kuendeleza utaalam na uwajibikaji katika maeneo yote.

2.3.2 Kuimarisha utamaduni wa uhuru wakijamii na kwa sababu hiyo kutupilia mbali sheria zote za ukandamizaji ambazo zinawanyima raia uhuru wao na kuleta serikali iliyo wazi na safi kwa njia ya kukosoana.

2.3.3 Kusaidia kuleta amani na haki kote ulimwenguni kwa njia ya vitendo na sheria kwa

kushirikiana na vyombo vya ndani na nje vinavyopigania kuondolewa kwa njia zote za ukandamizaji zinazofanywa kwa msingi ya rangi, kabila, au dini. Kwa sababu hii UDP itaunga mkono Tangazo la ulimwengu la haki za binadamu na mkataba wa nchi za umoja wa OAU wa haki za binadamu, na mapatano yote yanayofutilia mbali uonevu na mateso kwa binadamu.

2.3.4 Kuwashauri watu wote kujiunga katika shughuli za umma na ujenzi wa Taifa bila ubaguzi, na kwa mipango hii UDP haitafanya ubaguzi wowote ule dhidi ya binadamu, akina mama, watoto na vijana. Hili liwe ni kosa ambalo litapewa adhabu ya kisheria.

2.4 Maendeleo na Matumaini

2.4.1 Kuimairisha matumizi bora ya Urithi wa taifa letu, Ardhi ya Tanzania kwa njia ya mipango ya matumizi ya ardhi ya soko huria na mamlaka ya

binafsi.

2.4.2 Kuendeleza na kufuata mipango ya ulinzi wa mazingira hususani ardhi na wanyamapori wetu.

2.4.3 Kuimarisha uchumi ambao unavutia watu wanaotaka kuweka vitega uchumi nchini kwetu kwa njia ya soko huria, na kwa kusaidia mipango hii UDP itasaidia kuleta sheria zinazozuia kubanwabanwa kwa soko la hela, mipango, biashara, viwanda, utalii, kilimo na uchimbaji wa madini.

2.4.4 Kuboresha kilimo chetu kwa njia ya mipango inayosisitiza kilimo cha biashara na viwanda vinavyohusiana na mazao ya kilimo.

2.4.5 Kuendelea na kusaidia mikakati ya watu binafsi wanaotaka kujiendeleza ili kuboresha maisha yao, kwa makusudi haya UDP itaondelea mbali vizuizi kwa watu binafisi au kampuni zao kuweka vitega uchumi vyao, kufanya biashara au kukopa hapa nchini au nje, na itahakikisha kuwa leseni

zinatolewa kwa wote wanaoshughulikia maswala haya.

2.4.6 Kuboresha mipango yote ya nchi kwenye nyanja za usafiri wa ardhini, angani au majini kwa kutayarisha bajeti zinazopendelea mipango hii.

2.4.7 Kuboresha mipango ya Elimu na Afya kwa njia ya makusudi kabisa katika bajeti ili kodi na mapato ya walipa kodi yaelekezwe katika kunufaisha nyanja hizi, na kufuata mipango bora ya taifa ili kuboresha maisha ya raia.

2.5 Uwezo wa Wananchi

2.5.1 Kuendeleza aina ya serikali ambayo inasisitiza matumizi ya mapato na uwezo wa wananchi uwe chini ya mamlaka ya tawala za mitaa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wenyewe.

2.5.2 Kuimarisha aina ya serikali ambayo mgao wake wa madaraka unawapa uwezo zaidi na kujitegemea tawala za mikoa, wilaya na vijiji, kwa

ajili ya kuendeleza vizuri zaidi maendeleo yao.

SEHEMU YA 3

3.1 Uanachama.

Uanachama wa binafsi utakuwa wazi kwa watanzania wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

3.2 Kuandikishwa kwa Wanachama.

Wanachama wataandikishwa na tawi lolote la chama baada ya kulipa ada ya kiingilio na michango ya kila mwezi ambayo thamani yake itatolewa na Halmashauri kuu ya Taifa.

3.3 Haki na wajibu wa wanachama

3.3.1 Wanachama wote watakuwa na haki ya kuhudhuria mikutano ya chama, na kuwajibika kikamilifu katika shughuli za chama, kama vile

kupiga kura na kupigiwa kura, na kufuatia mwenendo wa kidemokrasia, watakuwa na haki ya kuwa na sauti ya kuweka mipango ya chama na kuitekeleza.

3.3.2 Wanachama wote watahitajiwa kutetea mipango na siasa ya chama na kusaidia maendeleo yake.

3.4 Ukomo wa Uanachama

Mwanachama yeyote atáacha kuwa mwanachama kwa kujiondoa mwenyewe, kufukuzwa, au kufariki.

SEHEMU YA 4

MUUNDO WA CHAMA

4.1 Tawi

4.1.1 Kila tawi litakuwa na wanachama

wasiopungua 10 ambao ndio wataunda tawi.

4.1.2 Mamlaka ya tawi yatakuwa yafuatayo:-

(a) Mkutano Mkuu wa tawi.

(b) Halmashauri ya Utendaji ya tawi.

4.1.3 Mamlaka ya tawi - umbo na wajibu;

(a) Mkutano mkuu wa tawi utawajumuisha wanachama wote wa tawi na utakuwa na wajibu ufuatao:-

(i) Kupokea na kushughulikia habari zote za kazi za tawi katika eneo lake.

(ii) Kuchagua wajumbe wa halmashauri ya utendaji ya tawi.

(iii) Kuchagua wajumbe wa halmashauri zingine ambazo zitatakiwa na mkutano mkuu, lakini wasizidi watu 10.

(iv) Kufikia uamuzi juu ya swala lolote litakaloletwa mbele yake na halmashauri ya utendaji.

(v) Mkutano mkuu utakutana angalau mara moja kwa mwaka.

(b) Halmashauri ya utendaji ya tawi itawajumuisha wafuatao:-

(i) Mwenyekiti.

(ii) Makamu Mwenyekiti

(iii) Katibu

(iv) Mweka Hazina.

(v) Katibu (akina mama).

(vi) Katibu (Umoja wa vijana).

(vii) Katibu (Baraza la Wazee).

(viii) Wajumbe wengine kama itakavyokubaliwa na mkutano mkuu.

(c) Wajibu wa Halmashauri ya utendaji ya tawi itakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuingiza wanachama wapya.

(ii) Kukitangaza chama.

(iii) Kutathimini na kufikia uamuzi juu ya njia za kuimarisha chama katika eneo lao.

(iv) Halmashauri ya utendaji ya tawi watakutana angalau mara tatu kwa mwaka.

(v) Muda wa Halmashauri ya utendaji utakuwa ni miaka 5.

(d) Kazi za viongozi wa tawi zitakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mwenyekiti

Mwenyekiti atasimamia mikutano yote ya chama na atakuwa msemaji mkuu wa chama.

(ii) Makamu Mwenyekiti

Atamsaidia mwenyekiti katika kuendesha na kusimamia kazi za kila siku za chama, na atakuwa badala ya mwenyekiti wakati ameondoka.

(iii) Katibu

Atatunza nyaraka zote za chama na ataweka kitabu cha kuandikishwa kwa wanachama, na kuona kila mwanachama anatimiza wajibu wake.

(iv) Makatibu (Vijana/Wanawake)

Watamsaidia katibu kuedesha ofisi ya chama kwa uadilifu kila mmoja na nafasi yake.

(v) Muda wa viongozi wa tawi utakuwa ni miaka 5.

4.2 Wilaya

4.2.1 **Matawi yote ya UDP, ambayo yatafunika jimbo la Uchaguzi la Bunge yatahesabiwa kuwa ni wilaya.**

4.2.2 **Mamlaka ya Wilaya yatakuwa kama ifuatavyo:-**

(a) Mkutano wa wajumbe wa wilaya.

(b) Halmashauri ya utendaji ya wilaya.

(c) Halmashauri Kuu ya wilaya.

4.2.3 Muundo na wajibu wa Mamlaka za Wilaya

(a) Mkutano wa wajumbe wa wilaya utawajumuisha wafuatao :-

(i) Wajumbe wote wa halmashauri ya utendaji ya wilaya.

(ii) Wajumbe wote wa halmashauri za utendaji za matawi.

(b) Wajibu wa mkutano wa wajumbe wa wilaya utakuwa kama ifuatavyo :-

(i) Kupokea na kushughulikia taarifa zote za shughuli za chama kutoka matawini.

(ii) Kuchagua wajumbe wa halmashauri ya utendaji ya wilaya.

(iii) Kuchagua wajumbe wa kamati zingine zitakazohitajika lakini wasizidi wajumbe watano kutoka kati ya wajumbe wa wilaya, ili kuhudhuria mikutano mikuu ya mkoa.

(iv) Kuchagua wajumbe wa kamati zingine zitakazohitajika lakini wasizidi wajumbe watano kutoka kati ya wajumbe wa wilaya, kuhudhuria mikutano mikuu ya taifa.

(v) Kuchagua wagombea viti vya bunge kwa jimbo la uchaguzi la wilaya.

(vi) Mkutano mkuu wa wilaya utakutana angalau mara moja kwa mwaka.

(c) Halmashauri ya utendaji ya wilaya itajumlisha wafuatao :-

(i) Mwenyekiti wa wilaya.

(ii) Makamu mwenyekiti wa wilaya.

(iii) Katibu.

(iv) Mweka Hazina.

(v) Katibu Mipango (Akina mama).

(vi) Katibu Mipango (Vijana).

(vii) Katibu wa Wazee.

(viii) Wajumbe wengine 5

waliochaguliwa chini ya kifungu **4.2.3 (a) iii - iv.**

(d) Wajibu wa halmashauri ya utendaji ya wilaya utakuwa kama ifuatavyo :-

(i) Kutathimini kazi za matawi na kutayarisha njia za kusaidia kuimarisha na kuendeleza mipango ya chama.

(ii) Kusimamia mipango ya mapato na matumizi ya matawi kuona kuwa inaendeshwa kwa manufaa ya chama.

(iii) Kufikiria na kutoa uamuzi juu ya swala lolote litakaloletwa mbele yake.

(iv) Halmashauri ya utendaji ya wilaya watakutana mara tatu kwa mwaka na muda wao wa kukaa madarakani utakuwa ni miaka mitano.

(e) Wajibu wa viongozi wa wilaya;

(i) Mwenyekiti

Atasimamia mikutano yote ya wilaya na atakuwa msemaji mkuu wa chama katika wilaya.

(ii) Makamu Mwenyekiti;

Kumsaidia mwenyekiti katika kazi zote za chama na kusimamia mikutano wakati mwenyekiti hayupo.

(iii) Katibu.

Atakuwa na wajibu juu ya shughuli zote za chama na atatunza nyaraka zote za chama na kuhakikisha kuwa mikutano inafanyika wakati itakiwapo.

(iv) Makatibu (Vijana na Wanawake).

Watamsaidia katibu kuendesha ofisi vizuri, na kila mmoja kulinda maendeleo ya sehemu

yake.

(v) Viongozi wa wilaya ndio watakaofanya Halmashauri Kuu ya wilaya. Halmashauri ya viongozi wa wilaya itashughulikia kazi zote za kila siku za UDP katika wilaya.

4.3 Mkoa

4.3.1 Mkoa utajumuisha wilaya zote za chama katika mkoa huo.

4.3.2 Mamlaka za mkoa yatakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu wa wajumbe wa mkoa.

(b) Mkutano wa halmashauri ya utendaji mkoa.

(c) Halmashauri ya uongozi mkoa

4.3.3 Muundo na wajibu wa mamlaka za mkoa :-

(a) Mkutano mkuu wa wajumbe mkoa utawajumlisha.

(i) Wajumbe wote wa kamati ya utendaji mkoa

(ii) Wajumbe wote wa kamati za utendaji wilaya

(b) Wajibu wa mkutano mkuu wa wajumbe wa mkoa itakuwa :-

(i) Kupokea na kutathimini taarifa zote za shughuli za chama kutoka wilayani.

(ii) Kuchagua wajumbe wa halmashauri ya utendaji mkoa.

(iii) Kuchagua mjumbe mmoja kuwakilisha mkoa katika kamati ya utendaji ya Taifa (NEC).

(iv) Kuchagua idadi ya wajumbe kama itakavyohitajika kwenye halmashauri zingine, lakini wasizidi watano kwa mkutano

mkuu wa Taifa na mkutano wa utendaji wa mkoa.

(v) Kuchagua idadi ya wajumbe kama itakavyohitajika kwenye halmashauri zingine, lakini wasizidi watano kwa ajili ya halmashauri ya utendaji ya mkoa.

(vi) Mkutano mkuu wa wajumbe wa mkoa watakutana angalau mara moja kwa mwaka.

(c) Halmashauri ya utendaji ya mkoa itajumuisha wafuatao :-

(i) Mwenyekiti wa mkoa.

(ii) Makamu mwenyekiti wa mkoa.

(iii) Mjumbe mmoja wa kamati ya utendaji ya Taifa.

(iv) Katibu wa mkoa.

(v)Mweka Hazina.

(vi)Katibu wa Mkoa mipango/Akina mama.

(vii)Katibu wa Mkoa mipango/Vijana.

(viii)Katibu wa Wazee.

(ix)Wajumbe wengine wa halmashauri waliochaguliwa na mkutano mkuu wa mkoa chini ya kifungu 4.3.3. (b) iv - v.

(d) Wajibu wa halmashauri ya utendaji ya mkoa utakuwa:-

(i)Kutathmini utendaji kazi wa wilaya na matawi na kutayarisha mipango ili kufanikisha mipango ya chama katika mkoa.

(ii) Kushughulikia na kutoa uamuzi juu ya maswala yatakayoletwa mbele yake na Halmashauri Kuu ya Mkoa.

(iii) Halmashauri ya utendaji ya mkoa itakutana angalau mara nne kwa mwaka, na watakuwa katika kazi kwa muda wa miaka (5) mitano.

(e) Wajibu wa viongozi wa mkoa:-

(i) Mwenyekiti

Mwenyekiti atasimamia mikutano yote ya chama,na atakuwa msemaji mkuu wa chama katika mkoa.

(ii) Makamu wa Mwenyekiti

Makamu wa Mwenyekiti atamsaidia mwenyekiti katika shughuli zote za siku hadi siku, na atasimamia mikutano wakati mwenyekiti asipokuwapo.

(iii) Katibu wa Mkoa

Katibu atawajibika katika maswala yote ya